MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA

TanTrade

**Programu ya mafunzo ya biashara ya Mpakani Tunduma/Nakonde 26-29 Juni 2023**

Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanznaia (TanTrade) kwa kushirnikiana na Kituo cha Kimataifa cha Biashara (ITC) inatekeleza mradi (*COMESA Cross Border Trade Initiative (CBTI)* wa kujenga uwezo wafanyabiashara wadogo 150 wanawake kwa wanaume na vijana wa mpakani Tunduma wanaojishughulisha biashara mbalimbali kupitia mpaka wa Tunduma wa Tanzania na Nakonde wa Zambia. Mafunzo hayo yanalenga kujenga uwezo wafanyabiashara hao ili kufahamu taratibu wa kuvusha bidhaa katika masoko ya kikanda hususani SADC na COMESA ambapo mpaka huo unahusika kutokana na kuwa lango la usafirishaji kwenda nchi zaidi ya 7 zilizo kusini mwa jangwa la Sahara.

Pamoja na kufahamu taratibu ni kuwezesha wafanyabaishara kufahamu fursa zilizopoa katika masoko ya kikanda, mahitaji ya bidhaa, urasimishaji biashara ya mpakani, matumizi ya mtandao katika biashara, haki na wajibu katika biashara ya mpakani na athali ya kutumia njia isiyorasmi mpakani na namna ya kuepuka manyanyaso katika biashara ya mpakani.

Mafunzo haya ni mwendelezo wa yaliyofanyika mwezi April 2022 ambapo kwa safari hii mafunzo yatafanyika tarehe 26 – 29 Juni, 2023 Tunduma, ambapo washiriki wa mafunzo hayo wanahitajika kujisajili kupitia Maafisa Biashara walipo Tunduma Mji. Wakufunzi wa mafunzi hayo wanatoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, TanTrade, Maafisa Biashara Tunduma, TCCIA Tunduma na Mkufunzi Mratibu wa Mradi kanda ya COMESA kutoka Zambia.

Manufaa ya mraji, ni pamoja na kuwezesha wafanuabaishara:-

a) Kuongeza uelewa na maarifa katika biashara ya mpakani;
b) Kupata taarifa za biashara ya nje kwa urahisi za haraka zaidi ili kufanya maamuzi sahihi;

c) Kupata usaidizi katika biashara ya mpakani pale ambapo unakumbana na changamoto za kibiashara;
d) Kurasimisha biashara ya mpakani kirahisi zaidi;
e) Kuongeza mauzo na kukua kwa biashara inayofanyika, na
f) Kujenga mazingiora wezesha kwa wafanyabiashara wa mpakani.